



MPANGO WAKUPIGA KURA

Uchaguzi wa Katikati ya Muhula 2026 | Novemba 3, 2026

⚠ Muhimu: Ni raia wa Marekani pekee wanaoweza kupiga kura. Ikiwa tayari wewe ni raia wa Marekani, mwongozo huu ni kwa ajili yako. Kura yako ni muhimu na ni ya siri. Hakuna mtu anayeweza kujua umempigia nani kura.

HATUA YA 1 | THIBITISHA USAJILI WAKO.

Hakikisha umesajiliwa kwa kutumia anwani yako ya sasa. Ikiwa umehama au umebadilisha jina, sasisha usajili wako. Tarehe za mwisho hutofautiana kulingana na jimbo.

Uthibitishe wapi? vote411.org au tovuti ya uchaguzi ya jimbo lako.



www.weall.vote/cws




[www.ballotpedia.org/
Sample_Ballot_Lookup](https://www.ballotpedia.org/Sample_Ballot_Lookup)



HATUA YA 2 | TAFUTA KARATASI YAKO YA KURA


Karatasi yako ya kura inategemea anwani yako kamili. Angalia mfano wa karatasi ya kura kabla ya siku ya uchaguzi ili ujue wagombea na nafasi zote zitakazopigiwa kura. Si lazima upige kura katika kila kinyang'anyiro.



HATUA YA 3 | JIFUNZE KUHUSU WAGOMBEA

Kabla ya kupiga kura, tafuta habari kuhusu wagombea na misimamo yao. Andika maelezo au leta orodha yako wakati wa kupiga kura. Unaweza kuleta nyaraka zako unapopiga kura.

Anza hapa: vote411.org | ballotpedia.org | Tovuti za wagombea





HATUA YA 4 | CHAGUA JINSI UTAKAVYOPIGA KURA

Majimbo mengi yanaruhusu kupiga kura mapema au kwa njia ya barua; si lazima usubiri Siku ya Uchaguzi.

Kura ya mapema ana kwa ana	Angalia tarehe ya kuanza katika jimbo lako.
Kura kwa barua	Omba karatasi yako ya kura mapema; tarehe za mwisho hutofautiana kulingana na jimbo.
Siku ya Uchaguzi	Novemba 3, 2026. Saa za kufungua hutofautiana kulingana na eneo.

 **Wapiga kura wa Oregon:** Oregon hupiga kura kwa njia ya barua pekee. Karatasi yako ya kura itatumwa kwako moja kwa moja.

HATUA YA 5 | PANGA SAFARI YAKO YA KUPIGA KURA

Tafuta mahali pa kupigia kura kabla ya Siku ya Uchaguzi. Panga jinsi utakavyofika. Ikiwa inahitajika, panga malezi ya watoto au muda wa kutoka kazini.

Tafuta mahali pa kupigia kura: vote411.org au tovuti ya uchaguzi ya jimbo lako.



VYA KUJA NAVYO SIKU YA UCHAGUZI

- ☐ • Kitambulisho halali chenye picha (kinahitajika katika majimbo mengi; angalia sheria za jimbo lako).
- ☐ • Mfano wa karatasi yako ya kura uliujaza au maelezo yako.
- ☐ • Kadi yako ya usajili wa mpiga kura (inahitajika katika baadhi ya majimbo).
- ☐ • Rafiki au mwanafamilia ambaye pia anaweza kupiga kura!

Nambari ya Msaada wa Ulinzi wa Uchaguzi:

 **866-OUR-VOTE (866-687-8683)**

Nambari hii ni ya bure kupiga simu na inapatikana kwa lugha mbalimbali.



UNAHITAJI MSAADA AU UNA MASWALI?

- Unahitaji msaada wa lugha? Muulize mhudumu wa uchaguzi. Sheria ya shirikisho inahitaji msaada wa lugha katika maeneo mengi.
- Unahitaji msaada wa kupiga kura? Unaweza kuja na mtu unayemchagua akusaidie.
- Jina lako halipo kwenye orodha? Omba karatasi ya kura ya muda (provisional ballot). Usiondoke bila kupiga kura.

Timu yako ya CWS ya ushiriki wa kiraia iko hapa kukusaidia!

Pata rasilimali zaidi kwenye:



[WWW.CWSGLOBAL.ORG/RISE-UP/](https://www.cwsglobal.org/RISE-UP/)

Rasilimali hii ni ya elimu ya kiraia isiyoegemea upande wowote. Rise Up for Refuge na CWS Global hawaungi mkono mgombea au chama chochote.